

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU**

SHULE YA SEKONDARI SUKUMA,
S.L.P 380,

MAGU

TAREHE 15/12/2020

Kumb Na SSSS/OG/.....

Jina la mwanafunzi.....

S.L.P

YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SUKUMA WILAYA YA MAGU MKOA WA MWANZA MWAKA 2021.

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuharifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari SUKUMA ipo umbali wa kilometra kumi na mbili (12) kutoka makao makuu ya wilaya ya Magu barabara ya kuelekea Kabilia (Ndagalu).

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shulenii kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 22/01/2021 (Baada ya tarehe 22/01/2021 hautapokelewa). Kuanzia tarehe 22/02/2020 patakuwepo na mtihani wa kupima uwezo wa mwanafunzi, hivyo jitahidi sana kuripoti kabla ya tarehe hiyo.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1. SARE ZA SHULE

(a) WASICHANA

(i) Sketi 2 ndefu linda boksi yenyelinda moja mbele, moja nyuma, malinda mawili kila upande kushoto na kulia rangi ya kijani mgomba. Pia iwe na belt la kawaida lisiwe kubwa. Sampuli ya kitambaa imeambatanishwa. Aje nazo shuleni kwa ajili ya uhakiki. Sketi ziwe ndefu Kuvuka magotii.

(ii) Mashati mawili meupe mikono mifupi. Aje nayo shuleni yote kwa ajiri ya uhakiki

(iii) Sweta aina ya pull over rangi ya kijani iliyokolea. Aje nayo shuleni kwa ajili ya uhakiki

(iv) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kufunika miguu, visivyo na urembo na visigino virefu (flat shoes) vinavyoruhusu kung'arishwa kwa rangi ya viatu na vyenye gidamu yaani vya kamba.

(v) Soksi nyeupe ndefu jozi 2 (stocking). Aje nazo shuleni kwa uhakiki

NB: Kwa waislamu rangi ya ijabu iwe nyeupe.

Tafadhari tumuomba sare za shule ziwe mpya na zifanane na kitambaa kilichoambatanishiwa.

(b) WAVULANA

(i) Suruari 2 rangi ya kijani mgomba upana wa chini uwe inchi 17, zenyе marinda ya mapanga mawili mawili kila upande; mifuko 2 pembedi na nyuma mfuko mmoja.

(Tafadhari modo haziruhusiwi). Aje nazо shulenі kwa uhakiki.

(ii) Shati mbili nyeupe mikono mifupi zinazofika kwenye kiwiko cha mikono. Aje nazо shulenі kwa uhakiki **(Tafadhari zisiwe modo).**

(ii) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kufunika miguu, visivyo na urembo na visigino virefu (flat shoes) vinavyoruhusu kung'arishwa kwa rangi ya viatu na vyenye gidamu yaani vya kamba.

(iii) Sweta aina ya pull over rangi ya kijani. Aje nayo shulenі kwa uhakiki.

(v) Soksi nyeupe fupi jozi 2. Aje nazо shulenі kwa uhakiki.

vi) Mkanda mweusi wa ngozi (usiwe wa tambi).

NB: Tufadhari tunaomba sare za shule ziwe mpya na zifanane na kitambaa kilichoanbatanishva.

C. SARE ZA MICHEZO

WASICHANA

(i) Tack suti rangi ya blue.

(ii) Raba na socks za michezo.

WAVULANA

i) Bukta rangi ya blue ya michezo.

ii) Raba na socks za michezo.

2.2 MAHITAJI MENGINE

- ❖ Counter book 12 quire 2 na daftari kubwa 12 kiwa ajili ya mazoezi.
- ❖ kalamu za wino wa blue, nyeusi na penseli.
- ❖ Mkebe mmoja wa hesabu (mathematical set).
- ❖ School bag nyeusi au mfüko wa kitambaa ulioshonwa rangi ya kijani ingomba
- ❖ Dictionary.
- ❖ Picha passport size 3 : picha zote zifanane.
- ❖ Vifaa vya usafi -mfagio wa chelewa wenye mpini na ndoo ndogo.

NB: Mzazi/mlezi tunapenda kukutaarifu kwamba mwanafunzi hatapokelewa shulenі bila kukamilisha mahitaji yote aliyoagizwa kuja nayo.

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu, sayansi , teknolojia na ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya RAISI-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shulenii.

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- (c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni.
- (d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifua maclekezo juu ya kuwèpo ndani na nje ya mipaka hiyo vakati wote wa uanafunzi wako katika shule hi.
- (f) Kutunza usafi wa mivili, mavazi na mazingira ya shule.
- (g) Kuвая sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- (h) Kutunza mali za umma.

3.2. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE:

- (i) wizi
- ii) uasherati na ushoga.
- (iii) Ubakaji
- (iv) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyaa kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika.
- v) Kupigana au kupiga.
- vi) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- vii) Kuwa mjamzito/ kupata mimba.
- viii) Kuoa au kuolewa.
- ix) Kutoa mimba.

x) Kugoma, kuchocha au kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

xi) Kukataa adhabu kwa makusudi.

xii) Kuwa na simu ya mkononi.

xiii) Kumiliki au kukutwa na vitu vyenye ncha kali kama kisu, sindano, pisipisi nk.

xiv) Kukwepa au kukataa kwa makusudi kufanya mitihani.

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.

- ❖ Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikari.Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti.
- ❖ Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- ❖ Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatayotolewa.

5.0 TAFADHARI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/ MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI SUKUMA
THOMAS Y PAUL

.....

MKUU WA SHULE

FOMU YA KUKUBALI NAFASI ULIYOPEWA

SEHEMU A: TAARIFA ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili.....
2. Tarehe ya kuzaliwa.....
3. Wilaya alipozaliwa.....
4. Kukubali nafasi ijazwe na mwanafunzi

Mimi Nimesoma maagizo yote ya kuijunga na shule ya sekondari na kukubali kutimiza masharti yote ya shule ikiwa ni pamoja na uletaji wa vifaa vinavyohitajika na kutii sheria zote za shule. Nitakapokuwa shulenii Sukuma sekondari nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kuzingatia yote ambayo wanafunzi wanatakiwa kutimiza katika suala zima la kupata elimu ya kujitegemea.

Sahihi ya mwanafunzi..... Tarehe.....

SEHEMU B: HABARI ZA WAZAZI/ MLEZI (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI)

1. Jina kamili.....
2. Ni mzazi au mlezi.....
3. Anwani yake.....
4. Kazi yake.....
5. namba tatu za simu ikiwemo ya mzazi/ mlezi na ndugu wa karibu
.....,,

UTHIBITISHO WA MZAZI/ MLEZI

Mimi mzazi/ mlezi wa nimesoma na kuhakikisha kwamba maagizo yameeleweka na motto wangu amejaza kikamilifu sehemu A

Pia nitahakikisha mwanangu anahudhuria shulenii kikamilifu bila kukosa vinginevyo nishitakiwe
Sahihi ya mzazi/mlezi..... Tarehe.....

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MAGU DISTRICT COUNCIL
REQUEST FOR MEDICAL SCHOOL EXAMINATION

Pupil's name.....

Age.....

Blood count (red & white).....

Stool.....

Urine.....

Syphilis test.....

T.B test.....

Eye test.....

Ears.....

Chest.....

Spleen.....

Abdomen.....

ANY ADDITION INFORMATION eg Physical defect chronic or family diseases etc

.....
.....
.....
.....
.....

Signature

Designation.....

Date.....

❖ Delete as necessary.